Mpendwa Mzazi au Mlezi,

Ili kuhakikisha mtoto wako yupo tayari kwenda shule, Sheria ya California, Kanuni ya Elimu Kifungu 49452.8, inahitaji mtoto wako atathminiwe afya ya kinywa (ukaguzi wa meno) ifikapo tarehe 31 Mei katika shule ya chekechea au darasa la kwanza, yoyote ambayo itaangukia mwaka wake wa kwanza katika shule ya umma. Tathmini ambazo zimefanyika miezi 12 kabla ya mtoto wako kuanza shule hutimiza sharti hili pia. Sheria inabainisha kwamba tathmini lazima ifanywe na daktari wa meno aliyeidhinishwa au mtaalamu mwingine aliyeidhinishwa au mtaalamu wa afya ya meno aliye sajiliwa.

**Tafadhali peleka fomu iliyo ambatanishwa ya Tathmini ya Afya ya Kinywa ya Shule ya Chekechea kwenye miadi ya Mganga wa meno wa mtoto wako, au mwambie mtoa huduma wako wa meno ajaze fomu ili kuthibitisha kuwa ukaguzi wa meno ulikamilika ndani ya miezi 12 baada ya mtoto wako kuanza shule. Ikiwa huwezi kumpeleka mtoto wako kwenye tathmini hii inayohitajika, tafadhali onyesha sababu juu ya hili kwenye Sehemu ya 3 ya fomu. Fomu zilizojazwa lazima zirudishwe shuleni kwa mtoto wako kabla ya tarehe 31 Mei.**

Ikiwa unahitaji msaada wa kutafuta mganga wa meno ili kukamilisha sharti hili, unaweza kuwasiliana na sehemu zifuatazo zilizo orodhesha hapa chini. Unaweza pia kurejea Orodha ya Kliniki za Meno za Jumuiya ya Kanda ya Mashariki iliyo ambatanishwa.

1. Medi-Cal kwa Familia/Denti-Cal: Simu #: 1-800-322-6384; au mtandaoni www.denti-cal.ca.gov 2.
2. San Diego Kids Health Assurance Network – Simu #: (619) 542-4039
3. 2-1-1 San Diego (Ikiwa huwezi kupata 2-1-1 kutoka simu ya mkono tafadhali tumia 858-300-1211)
4. Jumuiya ya Meno Kata ya San Diego – Simu: (619) 275-7188; au mtandaoni www.sdcds.org/

Mambo mengi, ikiwa ni pamoja na afya, huathiri maendeleo na mafanikio ya mtoto shuleni. Vishimo vinaweza kuzuilika, lakini huathiri watoto zaidi kuliko ugonjwa mwingine wowote sugu. Watoto wanahitaji meno yao kula vizuri, kuzungumza, kutabasamu, na kujisikia vizuri wao wenyewe. Kuoza meno ni maambukizi ambayo hayaponi na yanaweza kuleta uchungu ikiwa yataachwa bila matibabu. Ikiwa matundu hayatatibiwa, watoto wanaweza kulazwa hospitalini na meno yao ya kiutu uzima yanaweza kuharibika kabisa.

Sheria ya California inahitaji shule kudumisha usiri wa taarifa za afya ya mwanafunzi. Utambulisho wa mtoto wako hautohusishwa na ripoti yoyote itakayotolewa kutokana na sharti hili. Ikiwa una maswali kuhusu mahitaji ya Tathmini ya Afya ya Kinywa, tafadhali wasiliana na ofisi ya afya ya shule.

Kwa dhati,
Jennifer Shultz, MSN, RN ,SNSC

Jennifer Shultz (MSN,RN, SNSC) | Coordinator, Nursing & Health Services| shultzj@cajonvalley.net | P:619.588.3297 |F:619.588.3015